# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

**Telegrams: "SIASA"**
**Telephone: 026 2323525**
**Telephone: 022 2131070**
**Email: info@orpp.go.tz**

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi, Mtaa wa Nzuguni A .
S.L.P. 2851
41220 - **DODOMA.**

26 Septemba, 2025

**UJUMBE WA POLE**

Kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wote wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa natoa salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kufuatia kifo cha kaka yake mpendwa, Marehemu Abbas Ali Mwinyi kilichotokea jana huko Unguja, Zanzibar.

Vilevile, natoa pole kwa familia nzima ya Marehemu Mzee Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msiba huu mzito wa kuondokewa na ndugu yao. Pia, nawafariji wananchi wa Jimbo la Fuoni waliopoteza kiongozi na mpendwa wao.

Katika kipindi hiki cha majonzi, mimi pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa tunaungana na familia kwa sala na maombi, tukimuomba Mwenyezi Mungu awape wafiwa wote faraja, subira na nguvu ya kuvumilia msiba huu.

*"Sote ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake tutarejea."*

Jaji Francis S. K Mutungi
**MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**